

# Pambazuko


Toleo Namba 061

Jumatatu Februari 12-18 2024



## Bandari Mtwara kumekucha

● Yaanza kushughulikia shehena ya Msumbiji



TAHARIRI:

**Kifo cha Lowassa  
hakitaacha salama  
wanafiki**

**Kurasa 9 ndani  
maalum kumlilia**

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

## Tahariri

### Kifo cha Lowassa hakitaacha salama wanafiki

TANZANIA inaomboleza kifo cha aliyekuwa waziri mkuu wake, Edward Ngoyai Lowassa aliyeaga dunia juzi – Jumamosi, Februari 10, mwaka huu.

Kifo cha kiongozi huyo mahiri, mchapakazi, asiyeogopa kuchukua uamuzi mgumu, endapo una maslahi mapana kwa umma, kilitangazwa na Makamu wa Rais wa Tanzania Dkt. Philip Mpango.

Kufuatia kifo hicho, Rais Samia Suluhu Hassan ametangaza siku tano za maombolezo ya kitaifa na kwamba bendera zote zitapepea nusu mlingoti kuanzia siku ya kifo chake Februari 10, 2024 hadi Februari 14.

Baada ya dunia kujulishwa kifo cha Lowassa, Watanzania kwa mamilioni, wamejumuika – hasa kupitia mitandao, na viongozi wa nchi mbalimbali kutoa salamu nyingi za pole wakielezea kusikitishwa kuondoka kwa Lowassa kwenye uso wa dunia.

Pamoja na ukweli kwamba vilio vingi vimesikika, nyumbani kwa Lowassa huko Dar es Salaam na Monduli, lakini ukweli ni kwamba idadi kubwa ya watu wanamlilia mzalendo huyo wa Tanzania kupitia mitandao ya kijamii, hasa X, Facebook, Instagram na Tik Tok.

Vilio hivyo vya watu siyo bure, wanamlilia Lowassa kwa kuwa aligusa maisha yao akiwa madarakanina hata baada ya kuondoka kwenye utumishi wa umma.

Lowassa anaelezwa na kutangazwa na wengi kuwa alikuwa “mtu wa watu” aliyeugusa ustawi wa watu wengi kwa kuhakikisha wanakuwa na maisha bora – kupitia dhamana alizokuwa nazo.

Ni Lowassa ndiye “aliyevalia njuga” kuanzishwa kwa shule za sekondari za kata ambazo leo zinathibitishwa kuwa zilikuwa muhimu kwa kuwakomboa watoto kutoka kaya masikini. Kabla ya shule hizo, idadi kubwa ya vijana waliokuwa wakimaliza elimu ya msingi walibaki majumbani kwa ufynyu wa nafasi katika shule za sekondari, ambazo nyingi zilikuwa mijini tu.

Ni Lowassa aliyeamua binafsi kukomalia kuwepo kwa mtandao wa maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria kuwafikia majumbani wakazi wa Mwanza, Shinyanga, Tabora na sasa maji hayo yanaelekezwa hadi Dodoma.

Kazi nzuri za kujitua kwa Lowassa kutumikia umma, zipo nyingi na sehemu hii ya karatasi haitoshi kuzielezea. Hata hivyo, itoshe kusema kiongozi huyo alikuwa jemedari wa kung’ang’ania utekelezaji wa aliyoamini yatasaidia watu wa Tanzania kuukabili ufukara.

Hata hivyo, katika safari yake ya siasa na uongozi, pamoja na mzuri yote aliyoifanyia nchi hii, amekumbana na ‘visiki’ vingi mno ikiwamo kudhalilishwa na kutukanwa na watu wenye rika la watoto wake. Ni aibu, lakini hawa walifanya hivyo kwa ahadi za faranga ama dhamana ambazo wengine wanazo hadi leo.

Sisi katika Pambazuko tunaamini, wote waliomdhihaki Lowassa, hawatabaki salama, hata kama bado wako kwenye ukuu na huenda tukawaona wakilia zaidi siku ya kuaga mwili wa kiongozi huyo mahiri. Washindwe!

Alale salama Edward Ngoyai  
Lowassa.

## HALAFU IKAWAJE?...



*Makamu wa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, kushoto, akijadili jambo na watendaji wa Kituo cha Redio cha Wasafi, Jumatano iliyopita – Februari 7, ambapo alialikwa kuhojiwa, lakini kituo hicho kilizuiwa kumhoji kwa kile kinachodaiwa kuwa ni “maelekezo kutoka juu.” Hata hivyo, Nape Nnauye, waziri mwenye dhamana ya habari, alikanusha na kuhimiza vyombo vya habari kuacha kusingisia serikali kuhusu kuminya uhuru wa habari. Baadaye Wasafi waliibuka na kudai “kulitokea mkanganyiko wa ndani” na kusababisha kusitishwa kwa kipindi hicho. (Picha kutoka mtandao wa X).*

### Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

### **NUKUU**



*Mgombea binafsi ataimarisha vyama vya siasa na utawala bora, kwani upendeleo na kukata wagombea wanaoungwa mkono na wanachama kwenye kura za maoni utapungua. Pia wanawake wenye sifa hawatalazimishwa kugombea viti maalum kupisha wanaume majimboni – Prof. Anna Tibaijuka.*

## Tangazo

## Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

**Mhariri Mkuu,**  
**Oktoba, 2023**

## Changia Pambazuko liendelee

**WAJUMBE** wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukua Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yameweka wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata changamoto kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

**Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263**

Ukitema mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandaa: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchangia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscana



Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI



## **Bandari Mtwara kumekucha**

Na Mwandishi WETU

**M**TWARA sasa kumekucha; neema kwa wakazi wa mkoa huo imewafikia, huku makusanyo ya kodi yakiongezeka kupitia uwekezaji unaofanywa na serikali katika sekta ya bandari.

Kutokana na nia ya serikali ya kuhakikisha Bandari ya Mtwara inakua na kuimarika zaidi, nguvu kubwa ya fedha na utaalamu imewekwa ili kuifanya bandari hiyo kutumiwa na nchi jirani.

Tayari Msumbiji, baada ya bandari hiyo kuimarishwa, imeanza kuitumia kwa kupitisha shehena zake kwa kiasi kikubwa.

Pambazuko ambalo liliitembelea bandari hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita, lilishuhudia mabomba mengi ya mradi wa gesi nchini Msumbiji ambayo yemeteremshwa katika bandari ya Mtwara yakisubiri kusafirishwa kwa njia ya barabara kuelekea nchi hiyo jirani.

“Haya mabomba makubwa yaliyojazana hapa bandarini siyo ya Tanzania, yanapelekwa Msumbiji katika mradi wa usafirishaji gesi unaotekelezwa nchini humo...”

...Msafirishaji aliamua kuitumia bandari yetu baada ya kukosekana kwa amani katika eneo ambalo alipanga kwenda kuyashushia mabomba haya nchini Msumbiji,” anasema Meneja wa Bandari ya Mtwara, Ferdinand Nyathi.

Anaongeza; “Pamoja na kuwa ni kweli hali ya usalama ilimlazimisha msafirishaji kutumia bandari yetu, lakini ni ukweli pia kuwa maboresho yaliyofanyika hapa nayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kumfanya afikie uamuazi huo.”

Nyathi aliwaambia wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari waliotembelea bandari hiyo kuwa katika miaka ya hivi karibuni serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya kuboresha bandari hiyo na matunda yake yameanza



*Meli kubwa yenye urefu wa mita 210 ikipakia shehena ya korosho katika Bandari ya Mtwara kama ilivyoshuhudiwa na Pambazuko mwishoni mwa wili iliyopita. (Picha na Mpigapicha Wetu).*

kuonekana.

Anasema serikali iliamua kuwekeza hapo kwa sababu Bandari ya Mtwara inachukuliwa kuwa bandari ya kimkakati, kwani ina uwezo wa kuhudumia nchi kadhaa zinazoizunguka Tanzania zikiwemo Msumbiji, Malawi na Zambia.

Pia, ufanisi katika bandari hiyo unahitajika ili kuchechemua shughuli za ushoroba wa kusini wa uchumi ambao serikali imejikita kuuimarisha.

“Na sisi Bandari ya Mtwara tumeonesha kwa vitendo kuwa tunaweza kuifanya kazi hiyo ambayo serikali inataka ifanyike. Mathalan, baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuagiza kuwa korosho zote zinazozalishwa katika mikoa ya kusini zisafirishwe kwa kutumia bandari hii na siyo barabara, tumeweza kufanya hivyo kwani korosho zote zilizozalishwa katika msimu huu zimesafirishwa kupitia katika bandari licha ya changamoto chache za hapa na pale,” anasema Nyathi.

Ingawa Nyathi hakutaka kueleza kwa undani kuhusu changamoto hizo, lakini Pambazuko linafahamu kuwa baadhi ya wafanyabiashara wa korosho ambao walikuwa wanasafirisha zao hilo kwa

## Habari

### Bandari Mtwara kumekucha

*Inatoka Uk. 5*

njia ya barabara hadi Dar es Salaam hawakuridhishwa na uamuzi huo.

Wafanyabiashara hao wamekuwa wakifanya kila wanaloweza ili kukwamisha matumizi ya Bandari ya Mtwara kusafirishia korosho, lakini jitihada zao hizo zimegonga mwamba.

Kupitia uwekezaji huo bandari hiyo imeweza kujenga gati jipya la pili lenye urefu wa mita 300 na kina cha zaidi ya mita 13. Gati hilo lina uwezo wa kuhudumia meli zenye urefu wa zaidi ya mita 220.

Gati hilo pia limewekea mtambo wa kisasa wa kupakua na kupakia makasha (makontena) kwenye meli wenye uwezo wa kupakia au kushusha hadi makasha 30 kwa saa.

“Mtambo huu ulinunuliwa kwa Euro10.3 na hakika ni wa kisasa wenye uwezo mkubwa,” alisisitiza Nyathi na kuongeza: “Pamoja na uboreshaji huu uliofanyika, lakini wafanyabiashara hadi wa nje ya nchi wanavutika kuitumia bandari yetu kutokana na ufanisi mkubwa na gharama ndogo, ukilinganisha na bandari nyingine gharama za kuitumia bandari yetu hii, ni chini kwa wastani wa asilimia 30.”

Mkuu wa Idara ya Ubaharia katika Bandari ya Mtwara, Paul Muchwampaka, anasema kuna nafasi kubwa ya kuendeleza uwekezaji katika bandari hiyo kwani kuna maeneo mengi ambayo hayajaendelezwa.

Amelidokeza Pambauko kuwa kuna mpango wa kujenga mfumo mpya wa kupakia makaa ya mawe kwenye meli.

“Nafasi ya Bandari ya Mtwara kupanuka ni kubwa kwa sababu licha ya kuwa na maeneo makubwa ambayo bado hayajaendelezwa, lakini Mtwara ndio bandari inayoongoza kwa kuwa na mlango wa kuingingia bandarini wenye kila kirefu cha asili...”

“...Mlango wetu wa bandari hapa

katika eneo fupi una kina cha mita 50, katika maeneo mengine ya mlango yana kina hadi cha zaidi ya mita 100 na hiyo inatuweka katika nafasi ya kuwa na uwezo wa kuingiza meli yenye ukubwa wa aina yoyote ile bila matatizo,” anafafanua Muchwampaka.

Bandari ya Mtwara ilijengwa na wakoloni katika miaka ya 1950 ikiwa na gati moja lenye urefu wa mita 300 ikilenga kuingiza meli tatu kwa pamoja ambazo urefu wake hauzidi meta 100 kila moja.

Bandari hiyo ilitumika kwa ajili ya kusafirishia mazao ya kilimo kama vile karanga, korosho na mkonge.

#### Bandari yachoka lawama

Katika hatua nyingine inayolenga kuiondolea Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), lawama ambazo hazihusiani nazo, mamlaka hiyo imewaalika wadau wote wanaohusika na mnyororo wa usafirishaji shehena kwenda nje ya nchi na kuja nchini kupitia bandari kukutana na kujadili namna nzuri ya kuboresha huduma zake.

Kikao hicho kiatajadili na hatimaye kukubaliana viwango vya huduma kwa wateja ili kuwa na mfumo utakaoweza kila mdau kutekelea majukumu yake kwa kuzingatia makubaliano hayo.

Lengo la kukutana ni kukubaliana ili kuhakikisha kila mdau anatekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kufanikisha mnyororo wa usafirishaji na uingizaji shehena nchini.

Mkurugenzi wa Masoko wa TPA, Dkt. George Fasha, amesema mamlaka yake inafanya kazi na wadau zaidi ya 30, lakini mara nyingi inapotokea kasoro yoyote inayokwamisha usafirishaji wa mizigo kwenda nje ya nchi au kuingiza nchini, kidole cha lawama kwa kiasi kikubwa kinaelekezwa kwa TPA.



**Na Evarist Chahali**  
evarist@chahali.com

## Mezani kwa Chahali

### Tamu, chungu ya siasa alizopita Lowassa

Na Evarist CHAHALI

**J**UZI, Makamu wa Rais wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango aliwafahamisha Watanzania na dunia kwamba Waziri Mkuu wa zamani, Edward Lowassa amefariki dunia jijini Dar es Salaam.

Makala haya yanazungumzia matukio muhimu kuhusu Lowassa ambaye alishika nyadhifa mbalimbali serikalini na kisiasa.

Makala hayatazungumzia wasifu mrefu wa Lowassa, kwa sababu hilo limeshafanyika mara kadhaa hata kabla hajafariki.

Kadhalika, matukio yatakyotajwa katika makala haya ni yale tu ambayo mwandishi anaamini kuwa yanaweza kusaidia kuieleza hazina ya mwanasiasa huyo.

Lakini itakuwa vyema pia kutoa angalizo kabla ya kutaja matukio hayo, kwamba mila na desturi zetu zinakataza kuongelea mabaya ya marehemu. Hata hivyo, ni muhimu kuepuka “udikteta wa mila na desturi” hasa pale ambapo kuna haja ya kuweka kumbukumbu kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Kwahiyo, endapo baadhi ya matukio yatakyotajwa katika makala haya yatatafsiriwa kama “kumsema vibaya marehemu” basi ieleweke kuwa siyo kwa lengo baya.

Kabla ya 1995: Baada ya utumishi mrefu serikalini, Lowassa na aliyekuwa swahiba wake wakati huo, Jakaya Kikwete, walionesha dhamira ya kuutaka urais. Hata hivyo, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere aliweka pingamizi kwa sababu ambazo hazijawi kuwekwa hadharani.

Badala yao, chaguo la Nyerere lililikuwa Benjamin Mkapa ambaye alishinda urais mwaka 1995.

1995-2005: Lowassa na Kikwete waliunda kundi la kisiasa lililofahamika



*Edward Lowassa*

kama “Mtandao” likiwa na lengo la kuingia Ikulu baada ya Mkapa kumaliza muda wake. Wawili hao walifahamika kama Boyz II Men wakilinganishwa na kundi maarufu la muziki la nchini Marekani.

2005-2008: Ndoto za urais za wanasiasa hao wawili hao zilitimia na Kikwete alichaguliwa kuwa rais mwaka 2005 na akamteua Lowassa kuwa waziri wake mkuu. Hata hivyo miezi michache baada ya kushika wadhifa huo, serikali ya Kikwete ilikumbwa na kashfa maarufu ya Richmond, huko Lowassa akituhumiwa kuwa mhusika mkuu.

Februari 2008: Kufuatia kashfa hiyo, Lowassa alilazimika kujiuzulu.

2008-2010: kwa mujibu wa taarifa zisizo rasmi, inaelezwa kuwa kulikuwa na makubaliano kati ya Kikwete na Lowassa kwamba waziri mkuu huyo wa zamani “apokee kijiti cha urais” mwaka 2010. Hata hivyo, inadaiwa kuwa makubaliano mapya yalifikiwa kwamba Lowassa amwachie Kikwete amalize mihula miwili kisha yeye agombee mwaka 2015.

2010 - 2014: Lowassa alikuwa kama “rais anayesubiri tu muda wa kuapishwa” hapo 2015.

## Mezani kwa Chahali

### Tamu, chungu ya siasa alizopita Lowassa

*Inatoka Uk. 7*

2014 - 2015: Taarifa zinaeleza kuwa kulijitokeza mfarakano kati ya Kikwete na Lowassa ambaye alikuwa anasubiri tu swahiba wake amalize muhula wake wa pili kisha yeye aingie madarakani.

Kufuatia mfarakano huo, chaguo la Kikwete la mtu wa kumrithi likageuka kuwa Bernard Membe badala ya Lowassa.

2015: Licha ya tofauti zake na Kikwete, Lowassa aliendelea kampeni zake za kuwania urais kwa tiketi ya CCM huku mpinzani wake mkuu akiwa Membe.

Hata hivyo, ndoto zake za urais kupitia CCM zilifikia kikomo baada ya jina lake kuchujwa na chama hicho tawala, kupitia vikao ambavyo viliongozwa na Kikwete - mwenyekiti wa chama.

Bila kuchelewa, Lowassa akaamua kujiiondoa CCM na kujiunga na Chadema.

Wakati huo Chadema ilikuwa kwenye umoja wa vyama vinne, uliofahamika kama Ukawa, ambao uliafikiana kumsimamisha mgombea mmoja.

Ukawa ikampitisha Lowassa kuwa mgombea wake. Huko CCM, Membe aliishia kwenye “tano bora” na hatimaye chama hicho kilimpitisha John Magufuli kuwa mgombea wa urais kwa tiketi ya chama hicho.

Yayumkinika kutanabaisha kuwa Tanzania haijawahi kushuhudia mchuano mkali kwenye kinyang’anyiro cha urais kama ilivyokuwa kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, huku Lowassa na Magufuli wakionekana kuwa na takriban nafasi sawa za kuibuka washindi.

Hata hivyo, hatimaye Magufuli alishinda uchaguzi huo. Japo awali Lowassa alionesha kutoyatambua matokeo, baadaye suala hilo liliishia kimyakimya.

Moja ya mambo muhimu katika historia ya Tanzania, Chadema na Lowassa ambayo yayumkinika kusema “yamepuuzwa” ni swali hili: je ujio wa Lowassa huko Chadema ulikuwa ni faida ama ‘mzigo?

Swali la nyongeza, je, Chadema



*Edward Lowassa*

kufanya vibaya sana kwenye uchaguzi wa madiwani wa mwaka 2019 na kupoteza takriban viti vyote kwenye uchaguzi wa wabunge mwaka 2020 kuna uhusiano na ujio wa Lowassa kwenye chama hicho?

2019: Lowassa arudi CCM. Kimsingi, tangu mwaka 2018 kulianza kujitokeza dalili kwamba ni suala la muda tu kabla mwanasiasa huyo hajaachana na Chadema na kurudi CCM.

Hata hivyo, inadaiwa kuwa uamuzi wa Lowassa kurudi CCM ulichangiwa zaidi na misukosuko aliyokumbana nayo kutoka kwa serikali ya Magufuli hususan kwenye biashara zake mbalimbali.

Jumamosi Februari 10, 2024: waziri mkuu huyo wa zamani Lowassa afariki.

Kwa bahati mbaya – au pengine kwa makusudi – nafasi ya Lowassa katika siasa za Tanzania haikuongelewa sana wakati wa uhai wake, na kwa bahati mbaya, “udikteta wa mila na desturi zetu unaotaka kuongelea mazuri tu ya marehemu” unaweza kuwa kikwazo kwa wachambuzi kuangalia pande zote mbili za mwanasiasa huyo mkongwe, na ambaye kwa wakati fulani, alikuwa mwanasiasa maarufu kuliko yeyote nchini Tanzania.

Pumzika kwa amani marehemu Lowassa

*Barua pepe: evarist@chahali.com*





## Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

### Udhaliishaji huu kwa walimu haukubaliki

Na Rashid MTAGALUKA

**T**UKIO la walimu wa Shule ya Msingi Nyasalala iliyopo Kata ya Bukondo, Wilaya ya Geita, mkoani Geita, kukalia madaftari ya wanafunzi na wengine sakafuni, baada ya kamati ya shule hiyo kuwanyang'anya madawati waliyokuwa wakiyatumia ofisini kama mbadala wa meza na viti, linastahili kulaaniwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyosambaa kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii hivi karibuni, kamati hiyo ya shule ilikwenda na viongozi wa serikali ya kijiji wakiongozwa na mtendaji wa kijiji hicho ambaye hakutajwa.

Kwa vyovyote vile, tukio hili la kihuni lililofanywa na viongozi wa serikali iliyotarajiwa kuwaandalia viti, meza na vitendea kazi vingine watumishi wake hao wa idara ya elimu, halikubaliki katika jamii inayoishi kwenye nchi inayoheshimu utawala bora.

Binafsi nilitaraji viongozi wa serikali ya kijiji hicho wakiongozwa na ofisa mtendaji anayemwakilisha mkurugenzi wa halmashauri ya wilaya hiyo kabla haijachukua hatua ya kuwapokonya madawati na kuwapa wanafunzi, wangepata viti na meza kwanza!

Lakini, kitendo cha kuvamia shule bila hata kusaini kwenye daftari la wageni na kuamuru walimu wanyanyuke kwenye madawati waliyokalia huku wakitekeleza majukumu yao, siyo tu ni cha udhaliishaji, bali ni kuzorotesha maendeleo ya elimu yanayopiganiwa kila kukicha.

Sijui viongozi hao wa serikali ikithibitika wamehusika kwenye kadhia hii wanastahili kufanywa nini?

Hata hivyo, kilio na masikitiko yangu yako kwa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kinachoongozwa na Rais Leah Ulaya, kwa kushindwa kuwajengea ujasiri walimu kiasi cha kushindwa kujitetea.

Sote tunajua walimu ndiyo chemchem ya mafanikio ya taifa letu, hata rais wa



*Wasiri wa Elimu - Prof. Adolf Mkenda*

kwanza wa Tanzania, Julius Nyerere alikuwa mwalimu pale Sekondari Pugu, Pwani, sasa kwanini tunakubali kujenga na kustawisha utamaduni wa kubeza taaluma hii muhimu kiasi hiki?

Kitendo cha viongozi wa serikali kuwanyang'anya madawati waliyokuwa wakikalia walimu kutekeleza majukumu yao na kuyapeleka kwa wanafunzi, ni kuharibu haiba ya walimu mbele ya wananfunzi kwa upande mmoja, na kuwajengea wanafunzi kujiona ni bora kuliko walimu kwa ujumla wake!

Kwanini CWT hii inasahau jukumu lake la kuwajengea ujasiri wanachama wake ili kuepukana na vitendo 'haramu' vya kuinajisi taaluma ya ualimu mithili ya hivi vilivyofanywa na serikali ya kijiji iliyongozwa na ofisa mtendaji wa Nyasalala?

Hivyo basi, ni vyema ikafahamika kuwa walimu na jamii kwa ujumla wanayo imani kubwa na hivi vyama vya wafanyakazi kikiwemo CWT katika kulinda na kutetea maslahi mapana ya wanachama wake, lakini kikubwa vyama hivyo vioneshe kuwa vinawapa ari na ujasiri wa kujitetea kila wanachama wanapovamiwa na wahuni.

**\*Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari anapatikana kwa simu namba 0784 438546 au Barua pepe:mtagaluka@gmail.com**

## Kumbukizi

### Lowassa aliamua kupotea kunusuru wengine

Na Ansbert NGURUMO

**K**UNA watu wamekuwa wananitaka kijnjadili kile kilichoitwa ufisadi na usafi wa Edward Lowassa, katika muktadha wa orodha ya mafisadi 11 iliyotolewa na Chadema, Septemba 15, 2007, katika viwanja vya Mwembeyanga, Temeke, Dar es Salaam.

Wanataka kujua kwanini, baada ya yote hayo, Chadema ileile iliyojumuisha jina la Lowassa katika orodha hiyo, hatimaye ilimkaribisha na kumteua agombe urais mwaka 2015.

Kwa baadhi yao, nimekuwa natao majibu mafupi. Kwanza, nawashauri wapitie upya orodha ya mafisadi, wasome na kujikumbusha tuhuma za Chadema kwa kila mtuhumiwa.

Lowassa aliwekwa katika orodha hiyo kwa sababu alivunja mkataba wa kampuni ya City Water ya Dar es Salaam. Kampuni ilipeleka shauri mahakamani kudai fidia.

Chadema ilimshutumu Lowassa kwa uamuzi huo ambao, kwa macho yetu wakati ule, ulikuwa wa kibabe, na ungesababishia taifa hasara iwapo serikali ingeshindwa mahakamani.

Lowassa ana bahati. Serikali ilishinda shauri hilo. Kwa mantiki hiyo, ufisadi aliotuhumiwa Mwembeyanga ulifutika wenyewe mahakamani.

Lakini alikuwa na bahati mbaya, kwamba nguvu iliyokuwa imetumika kutangaza “ufisadi” huo mwaka 2007, haikutumika tena kutangaza “ushindi wake” mahakamani.

Akiwa ndani ya kikao kimojawapo cha Halmashauri Kuu ya CCM mwaka 2012, Lowassa alitumia ushindi wake huu kumkabili Rais Jakaya Kikwete alipoleta hoja ya mafisadi mbele ya wajumbe.

Kwa mara ya kwanza, baada ya kukaa kinyasi kwa miaka minne, Lowassa alipata ujasiri wa kumweleza Rais Kikwete kuwa miongoni mwa waliotajwa kwa ufisadi katika orodha ile, na Kikwete



Edward Lowassa

alikuwemo, lakini alikuwa hajasafishwa na kikao chochote au mahakama yoyote.

Ni jambo la bahati mbaya kwamba wananchi wengi wanaojadili orodha ya mafisadi, wanakosea kudhani na kusema kwamba Chadema ilimtuhumu Lowassa kwa ufisadi wa Richmond. Hapana! Ufisadi wake wa Mwembeyanga ulitokana na yeye kuvunja mkataba wa City Water.

Hata sakata la Richmond lilipoibuka mwaka 2008, likamuimiza Lowassa kisiasa na kijamii, Rais Kikwete, kwa kuwa alijua ukweli halisi, alimfariji Lowassa kuwa ile ilikuwa “ajali ya kisiasa.” Baadhi yetu tulikuwa hatujajua vyema undani wa sakata la Richmond.

Hata leo, wapo watu wanaodhani kwamba Richmond ilikuwa mali ya Lowassa.

Mwaka 2009, niliporejea nyumbani kutoka masomoni Uingereza, miongoni mwa watu wa kwanza niliokutana nao ni Dkt. Harrison Mwakyembe, mbumbe wa Kyela, ambaye pia ndiye alikuwa ameongoza kamati teule ya Bunge iliyochunguza sakata la Richmond.

Katika ushirika wetu wa kupambana na ufisadi, Dkt. Mwakyembe alikuwa rafiki yangu. Jioni moja, tukiwa nyumbani kwake Kunduchi, Dar es Salaam, tulizungumza mambo mengi ya kitaifa.

Dkt. Mwakyembe aliniambia kuwa kilichomponza Lowassa katika Richmond

## **Lowassa aliamua kupotea kunusuru wengine**

siyo umiliki, bali akiwa waziri mkuu alishiriki katika kusimamia mchakato wa kampuni hiyo kupewa tenda.

Aliniambia pia kwamba kamati teule ilipoanza uchunguzi, katika siku za awali kabisa, iligundua kuwa viongozi wa juu kabisa walikuwa wanahusika, lakini iliogopa kuwahusisha au kuwataja kwa kuwa wajumbe walihofia mambo mengi.

Aliongeza pia kuwa walikwepa kumhoji waziri mkuu Lowassa makusudi, kwani walitambua kuwa kwa cheo chake na utendaji wake, angeweza kuathiri matokeo ya kazi ya kamati kabla haijawasilishwa bungeni.

Lengo lao lilikuwa kumwadhibu waziri mkuu, kwa kuwa waliona “mkono” wake, hata kama hakuwa mmiliki.

Sababu kuu ya Dkt. Mwakymbembe na wenzake kumwadhibu Lowassa ni ugomvi wa madaraka bungeni kati ya Lowassa (waziri mkuu na kiongozi wa shughuli za serikali bungeni) na Samuel Sitta (spika). Nimewahi kueleza kuwa “ugomvi” wao ulisababishwa na ahadi ya Kikwete wakati anagombea urais.

Aliahidi kumpa Sitta uwaziri mkuu. Vilevile, aliahidi kuwapa wengine nafasi hiyohiyo, akiwemo Lowassa.

Baada ya uchaguzi, wakati anaanza kuunda serikali, huku Pius Msekwa akiwa ameshajiandaa kugombea uspika, Rais Kikwete alituma ujumbe wa kushtukiza kwa Sitta kumwomba agombea uspika!

Maelezo ya Rais Kikwete kwa Sitta ni kwamba, kwa kuwa walikuwa wamefanikiwa kukamata serikali, lakini hawakuwa na uhakika na bunge, alihitajika mtu wanayemwamini, awasaidie kukamata bunge, ili mambo yao yaende sawasawa.

Kikwete alimwaminisha Sitta kwamba hakuwa na mtu mwingine aliyeaminiwa kukamata bunge. Kwa ujumbe huo pekee, Sitta alijua kuwa hakuwa tena chaguo la Kikwete katika

uwaziri mkuu.

Zilianza kampeni kali kumsaidia Sitta, wakisaidiwa mno na vyombo vya habari. Msekwa alitwa “agano la kale.” Naye kwa kutojua, alimuuliza Rais Kikwete, “nasikia hunitaki?” Rais Kikwete anadaiwa kuwa alikanusha kuhusika na njama hizo.

Matokeo ya uchaguzi wa spika yalimpa ushindi Sitta. Lakini katika moyo na akili zake, hakuwahi kudhani kwamba Lowassa ndiye angetuliwa kuwa waziri mkuu.

Licha ya kwamba Sitta na Lowassa walikuwa kwenye kambi moja wakati wa kampeni, yeye na baadhi ya wenzake walikuwa wameanza kumzunguka Lowassa, kwa propaganda za mwaka 1995, kwamba “alikataliwa na Mwalimu Nyerere.”

Kwa hiyo, hata alipopokea barua ya uteuzi wa waziri mkuu kutoka Ikulu, Sitta alipatwa na mshtuko alipoona jina la Lowassa na kulisoma kwa wabunge ili wapige kura ya kumthibitisha.

Muda mfupi kabla ya hapo, mbunge mmoja mpya, aliyekuwa katika kambi ya Sitta, ambaye hakupenda Lowassa awe waziri mkuu, baada ya kupata tetesi kuwa Lowassa ndiye alikuwa chaguo la Kikwete, alikimbilia kwa Mzee Samwel Malecela, aliyewahi kuwa waziri mkuu, kumwomba asaidie kuzuia uwaziri mkuu wa Lowassa.

Akamwambia Malecela: “Nasikia atamteua Lowassa. Wewe uliondolewa kwenye kinyang’anyiro cha urais kwa sababu walisema Nyerere alikukataa. Nyerere huyohuyo si alimkataa na Lowassa? Tunataka utasaidie kufanya kampeni ya kupiga kura ya hapana, iwapo Lowassa atateuliwa.”

Mzee Malecela alimtazama mbunge huyo, akatabasamu, halafu akamwambia: “Sikiliza. Namjua Lowassa. Alipoteuliwa kuwa waziri kwa mara ya kwanza, aliletwa ofisini kwangu, katika Ofisi ya

## Kumbukizi

### Lowassa aliamua kupotea kunusuru wengine

Inatoka Uk. 11

Waziri Mkuu, akawa waziri wa nchi. Mimi ndiye nilikuwa waziri mkuu. Najua utendaji wa Lowassa. Ni mtu ambaye akiamua kufanya jambo, hataki kulala mpaka jambo hilo litekelezwe. Ni mchapakazi.

“Yote yatasemwa juu yake, lakini natambua kuwa akiwa waziri mkuu, atachapa kazi bila kupumzika. Pili, wewe naona ni mbunge mpya. Hujui watu hawa. Wameshashinda, na wameshika serikali. Utawapinga, lakini hutafaulu kuwazuia. Na ukishashindwa, ujue kuwa ubunge wako utakuwa wa tabu, kwa sababu watakuandama. Waache. Hutaweza kuzuia Lowassa kuwa waziri mkuu.”

Mbunge huyo aliondoka akiwa ameinamisha kichwa. Mbunge huyo, akiwa swahiba wa Sitta, alikuwa miongoni mwa wabunge machachari waliokuwa wanasumbua serikali bungeni. Zaidi ya hayo, alishiriki hata kuandika upya kanuni za bunge ili kuwezesha bunge libane serikali.

Kwake, serikali ilikuwa Lowassa, si Kikwete. Na lilipozuka suala la Richmond, kampuni iliyoingizwa nchini na Sitta akiwa mkurugenzi mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania, mbunge huyo aliteuliwa kuwa mjumbe katika kamati teule ya Bunge iliyochunguza sakata hilo.

Jambo ambalo halikujulikana mapema ni kwamba Dkt. Mwakyembe naye alikuwa akidaiwa kuwa mmoja wa wamiliki wa kampuni ya kuzalisha umeme, ikishindana na Richmond. Kwa hiyo, hakustahili kuwa mwenyekiti wa kamati teule, kwa kuwa na maslahi ya moja kwa moja. Ilikuwa lazima Lowassa “asulibiwe.” Kwao, ilikuwa zaidi ya Richmond.

Ilijulikana baadaye kwamba Lowassa hakujua kwamba Rais Kikwete alikuwa ameamua kujivua lawama katika

sakata la Richmond. Mara baada ya Bunge kuahirishwa mchana, Lowassa alikwenda moja kwa moja kwa rais. Wakateta kuhusu suala hilo, na jinsi bunge lilivyochafuka.

Rais akamshauri Lowassa ajiuzulu bungeni, lakini kwa ahadi kwamba angekataa barua yake ya kujiuzulu – ilimradi ameshaonesha moyo wa uwajibikaji. Vyanzo vya kuaminika vinasema Lowassa aliomba karatasi palepale, akaandika na kumpa karani aichape, baadaye akaisaini na kumkabidhi rais.

Mara tu alipoondoka Ikulu kuelekea Bungeni, ujumbe wa wabunge wa CCM ukaingia Ikulu wa rais na kumweleza kuwa kwa jinsi ilivyo, rais akimng’ang’ania Lowassa naye atanguka.

Muda mfupi baadaye ukaja ujumbe kutoka idara kadhaa za usalama, ukiwa na hoja hiyohiyo, kwamba asipoondoka Lowassa wabunge wanaweza kupoteza imani na rais.

Laiti Lowassa angejua kinachoendelea, angetumia fursa hiyo kujenga hoja na kujitetea bungeni. Alipokuja kujua, alikuwa ameshachelewa.

Ndivyo alivyopatikana Mizengo Pinda, na ndivyo Rais Kikwete alivyopata ujasiri wa kumpa pole Lowassa kwa kile alichaita “ajali ya kisiasa.”

Pamoja na hayo, Lowassa aliendelea kumfichia rais siri. Aliendelea kumwamini na kumlinda kwa kukaa kimya hata aliposhambuliwa.

Alivunja ukimya mwaka 2012 ndani ya kikao cha NEC alipotaka rais aeleze wajumbe ukweli kuhusu Richmond. Upepo ulichafuka kwa muda, lakini baadaye kikao kiliendelea bila rais kutoa ufafanuzi.

Kwa Lowassa, huo ulikuwa ushindi mkubwa uliompata ushujaa wa ghafla ndani ya NEC. Waliokuwa hawajui wakapata fursa ya kujua kwamba katika sakata la Richmond, yeye alipotea ili wengine wanusurike.

## Watendaji kutowajibika chanzo cha umasikini

Na Jesse KWAYU

**H**ALI ya miundombinu katika mikoa ambayo imepitiwa na mvua kubwa za hivi karibuni ni mbaya.

Barabara nyingi, hasa za changarawe na udongo, zina hali mbaya zaidi. Hata za lami kuna sehemu zimeharibika, yakiwamo madaraja madogo na makubwa.

Katika Jiji la Dar es Salaam ambalo kulingana na sensa ya watu na makazi ndilo bado linaongoza kwa kuwa na idadi kubwa zaidi ya watu nchini, hali ni mbaya zaidi.

Kwa mujibu wa ripoti ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, Dar es Salaam ndiyo mkoa unaoongoza kwa idadi ya watu ukiwa na wakazi 5,383,728 ukifuatiwa na mkoa wa Mwanza wenye wakazi 3,699,872.

Hapana shaka, hata mchango wa mikoa kwa uchumi wa taifa unafungamana sana na wingi wa watu ambao huakisi pia shughuli za kiuchumi hasa kwa wale wanaoishi maeneo ya mijini.

Hakuna ubishi kwamba nguvu kubwa sana ya fedha itahitajika kurudisha miundombinu iliyoharibika katika hali yake ya awali, ili kusaidia mawasiliano. Lakini kubwa ni kurejesha shughuli za kiuchumi katika hali yake ya kawaida.

Yapo baadhi ya maeneo watu wamepoteza wapendwa wao, nyumba zao, mashamba yao na mali nyingi kutokana na athari za mvua hizi ambazo zimesababisha mafuriko katika maeneo mengi ya nchi hii. Nawapa pole wote waliopoteza wapendwa wao na mali zao pia.

Inaeleweka kwamba mvua za kupitiliza kiasi ni maafa. Hakuna mtu anayeandaa maafa ya asili kama mafuriko. Hizi ni kudra za Mwenzi Mungu.

Hata hivyo, binadamu kwa kutumia maarifa ya kisayansi ana uwezo wa kupunguza kiwango cha madhara ya



*Mafuriko yanayosababishwa na kutowajibika kwa watendaji*

maafa haya. Hii ni pamoja na kuwa na taarifa sahihi na kuchukua hatua za tahadhari kwa wakati.

Kwa mfano, ingeliwezekana kabisa kuwaondoa kwa nguvu watu wote waliojenga na kuishi mabondeni, kwenye kingo za mito na maeneo yote ambayo kwa asili ni mapito na mkusanyiko wa maji – mabwawa.

Pamoja na uwezo huo, pia kuna suala la ubora wa ujenzi miundombinu yetu. Kwa mfano mpaka leo ni vigumu kuelewa inakuwaje mhandisi anajenga barabara isiyo na mitaro ya kuondosha maji ya mvua barabarani?

Inakuwaje mhandishi wa ujenzi wa barabara anapitisha barabara mtoni kabisa yanakopita maji ya mto? Inakuwaje kwa mfano miaka na miaka, mafuriko yatokee sehemu ile ile, lakini wenye wajibu wa kuepusha hali hiyo kwa kubuni miundiombinu bora zaidi hawafanyi lolote?

Nitaje Mkoa wa Dar es Salaam kama mfano – eneo la Jangwani. Hivi ni nani asiyejua kwamba kwa mpango na utekelezaji haitawezekana tena eneo lile kuwa salama kwa wakazi wa jiji hilo wakati wa mvua?

Ni dhadhiri kwa zaidi ya miaka 10 sasa imekwisha kuthibitika kuwa pale Jangwani kunahitajika suluhisho la maana la kitaalam.

Kwamba hakuna sababu hata moja ya magari na hata waenda kwa

## Makala

## Watendaji kutowajibika chanzo cha umasikini

Inatoka Uk. 13

miguu kwenda mpaka kwenye ukingo wa Mto Msimbazi ndipo wavuke. Haitawezekana. Imethibitika kuwa hilo kwa sasa halitawezekana tena. Lakini ni nani anayewaza kama pale Jangwani palipaswa pawe pameshajengwa daraja kubwa kuanzia Magomeni mpaka eneo la Fire?

Tatizo kubwa la nchi yetu ni uwajibikaji. Yaani wakubwa wanaweza kufanya uamuzi wa ajabu, wakatumia mabilioni ya fedha za umma kutekeleza mradi mkubwa ambao haukufanyiwa tathmini ya kutosha juu ya uimara wake na uhimilivu kutokana na madhara mengine ya kimazingira.

Ni katika 'ulevi' wa ukubwa kama huo tulishuhudia karakana kuu ya mabasi ya mwendo kasi ikijengwa Jangwani. Yaani mtoni kabisa! Na madhara yalipotokea kwa mabasi mengi kujaa maji baada ya karakana hiyo kufurika maji, hakuna aliyewajibika. Hakuna.

Ukitembea kwenye barabara nyingi za nchi hii, suala la utaalamu katika ujenzi wa barabara halizingatiwi kabisa. Barabara zinajengwa mpaka mtoni, mitaro ya maji ya mvua inaachwa kujengwa, kwenye miinuko mikali inaachwa hivyo hivyo, kwenye kona hatarishi vivyo hivyo.

Ipo mifano hai mingi tu. Jaribu kufikiria barabara kuu ya nchi hii, Barabara ya Morogoro, ile kona pale Kimara Mwisho mara tu baada ya kituo cha mabasi ya BRT, ni ya nini? Nini kilizuia kunyoosha ile barabara na kuepusha kero na hatari ya kona ile?

Kulikuwa na gharama gani ya kushindikana kubekka ili barabara pale inyooshwe? Hao wahandisi waliopitisha hiyo michoro walisahau kuwa hiyo barabara ndiyo inabeba malori karibu yote yanayotoka na kuingia bandari ya Dar es Salaam?

Hakuna anayeweza kuelewa kwamba wahandisi wetu wanasoma kanuni zilezile za ujenzi kama wa nchi nyingine,



*Mafundi wakhangaika na kuxibua kingo za Mto Msimbazi unaojaa maji kila mara*

lakini wanapokuja kutekeleza kazi zao, wanaamua kupigwa 'upofu' kiasi cha kusahau kabisa misingi ya ubora wa kazi zao.

Kuna mtu mmoja alitoa ushuhuda mahali akisema, siyo kila masikini ni mtu mvivu. Wapo wanaofanya kazi kwa nguvu sana, lakini hawajikwamui walipo kwa sababu wamejifunga katika mnyororo fulani.

Sisi kama taifa kwa kushindwa kufuata misingi bora ya ujenzi wa barabara na miundombinu mingine, tunajikuta mwaka baada ya mwaka tukiwa palepale tukishughulika na jambo lilelile kwa gharama kubwa.

Hatupigia hatua. Tunajifunga kwenye mnyororo wa umasikini, kwa kupuuzwa tu kanuni za ujenzi.

Jaribu kufikiria eti pale Jangwani siku hizi kuna mitambo ya ujenzi – vijiko, magreda, ambayo imepiga kambi wakati wote kusubiri kutoa mchanga na matope wakati wa mafuriko.

Hivi ile mitambo pale ni ya nani? Nani analipa gharama zake? Kwa nini imekuwa ni kazi ya kudumu? Kwa nini barabara ile isifumuliwe na kunyanyuliwa juu ili kuepuka yale maigizo ya kujilipa fedha za umma kwa kundoa mchanga mtoni? Umasikini mwingine tunajitakia wenyewe!

*Mwandishi wa makala haya ni mhariri msoefu na mmoja wa wakurugenzi wa Kampuni ya Media Brains, Dar es Salaam.*

## Namlilia Thadei, mwamba wa fikra huru

Na Luqman MALOTO

**U**LIMWENGU ni jukwaa la mateso kwa watu huru wene fikra huru, wenye kutumia akili zao kupokea, kutafsiri na kujenga hoja.

Ni dunia ya mateso kwa wanaounda mitazamo na misimamo baada ya kujiridhisha kwa tafakuri binafsi.

“Msingi wa fikra huru hauegemei katika nini unafikiri, bali kwa jinsi unavyofikiri ;” ndivyo anavyosema mwandishi wa Uingereza, Chris Hitchens.

Ni hakika kwamba, watu wenye kujitegemea kifikra na kuamua kufuata jambo kwa utashi wa fikra binafsi, mara nyingi hugeuka wapweke.

Upo wakati unapofikiri tofauti wa wengine. Utajikuta upo peke yako. Siyo ajabu ukazodolewa, hivyo kuifanya dunia kuwa ngumu upande wako.

Dunia ni nyepesi kwa wafuata mkumbo. Upepo unapovuma na wao wanaunga. Hawaumizi kichwa, wakisia mayowe wanafuata.

Fulani akisema jambo, bila hata kufanya tafakuri na hata kulichambua, naye naye anaamini hata kama huyo msemaji ni kizabizabina. Huu ni uchawa!

Thadei Ole Mushi, mwalimu kitaaluma, pia mwandishi huru, na mmoja wa wajenga hoja murua ninaowafahamu na kuwatambua.

Soma makala za Thadei. Andiko kwa andiko, utabaini kuwa katika ‘posti’ zake amekuwa akijenga hoja na misingi aliyosimamia. Thadei ni mantiki ya fikra huru.

Hakuona aibu kujisema yeye ni kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM). Hata sare za chama alivaa. Shughuli za CCM alishiriki waziwazi.

Lakini, kwa uwazi uleule, alikosea serikali na chama chake tawala. Ni kwa sababu msingi wa fikra zake, haukuegemea alichofikiri, bali jinsi alivyofikiri.

Tembelea akaunti zake; iwe Facebook, X, Instagram, soma posti kwa posti. Kuna mahali akiandika, watu kwa wingi wao, walimpongeza. Kwingine alijenga hoja, watu kwa wingi kabisa walimshambulia, walimpinga na kumpa majina mabaya. Hiyo ndiyo gharama ya kuushughulisha ubongo kwa utofauti.

Abraham Lincoln, aliyewahi kuwa Rais wa Marekani, alifundisha kusimamia unachokiamini, hata kama kila mtu anafuata mkumbo.

Ni somo zuri, ila linaweza kusababisha ugonjwa wa moyo. Fikiria unauona ukweli ambao kila mtu hauoni. Halafu wewe mwenye ukweli, unaitwa majina mabaya.

Nilifahamu Thadei alikuwa katika hali ya kupigania maisha yake kutokana na maradhi yanayoelezwa kuwa ni moyo. Nilijua angenyanyuka akiwa imara, lakini sasa pumzi yake imekoma na nikapokea habari kuwa Thadei amepumzika. Sikuamini. Binadamu hatujawahi kukikubali kifo.

Kwangu, Thadei ni shujaa wa ufikiri huru.


Alale salama, Thadei ole Mushi.

Makala haya ya tanzia yamehaririwa kidogo kutimiza matakwa ya sera ya uhari ya gazeti la Pambazuko.



## Kitabu

Bei sh 45,000/=  
DAR: Free delivery  
Mikoani: delivery  
sh 5,000/=



M-Pesa 0767-340-975  
jina Anna



Instagram: @evarist\_chahali

Twitter: @chahali

TikTok: @j.a.s.u.s.i

[www.baruayachahali.com](http://www.baruayachahali.com)



## **Kwanini Lowassa alikuwa jive kwenye maji?**

Na Maggid MJENGWA

**E**DWARD Ngoyai Lowassa hatunaye. Ametangulia mbele za haki.

Kwa tunaosoma historia na kufuatilia siasa za Tanzania, tunajua, kuwa Edward Lowassa alikuwa ni mwanasiasa wa misimu yote.

Edward alikuwa na kuishi kwenye siasa. Lowassa miongoni mwa sifa zake nyingi, alikuwa 'bingwa' wa siasa za kimikakati na 'fundi' wa siasa za majukwaani.

Lowassa alijua asema nini na wapi asema alichotaka kusema. Alijua avae nini pia kulingana na hadhira yake.

Kwenye hilo la mwisho, kuna siku miaka ile nikiwa mwanasafu katika gazeti la Rai 'Nguvu ya Hoja,' Kaka yangu, Mhariri Johnsson Mwambo kwenye mazungumzo ya ana kwa ana akaniambia;

"Edward amenipigia simu kuniomba siku nyingine, kwenye habari zake kama waziri mkuu, tutumie picha zake akiwa na kofia ya pama badala ya suti na tai!"

Inatafakarisha. Ni kwa vile Waziri Mkuu Lowassa ameomba 'hisani' ya mhariri. Basi, Mhariri Mbwambo na mimi tulielewa, kuwa Lowassa, kimkakati, alitaka aonekane kuwa anafana na anaowaongoza. Yu karibu nao.

Lowassa kimsingi ni 'fundi' wa kusomea juu ya sanaa ya mwonekano jukwaani. Lowassa alijua, kuwa kwa mwanasiasa, hata ukisimama barazani kwako ukaonea na wapita njia, hilo ni jukwaa.

Kwa mwanasiasa, popote unaponekana ni 'jukwaa.' Swali la kujiuliza unaonekanaje kwa watu wako ukiwa jukwaani?

Ilivyo, watu wako wangependa pia wakuone umetinga suti na tai unapokutana na wageni wa kimataifa au kuhutubia mikutano ya kimataifa, kama ni mwanamme. Na kama ni mwanamke, basi, uvae vazi la kupendeza, na siyo



*Edward Lowassa akisalimiana na John Magufuli (kulia) ambaye alikuwa Rais wa Awamu ya Ne ya Tanzania. (Picha kutoka mtandao wa intaneti).*

sare inayofanana na wanayovaa wao.

Msingi wake ni kwamba, kila ulipo, una vionjo vya wale unaowawakilisha. Kuna mahali wangependa ufanane nao, na kuna mahali wangependa ufanane na wengine unaokutana nao, au kuwahutubia. Kujua ni wakati gani na wapi kivaliwe nini na kisemwe kipi; wanasiasa aina ya Edward Lowassa walijua hilo.

Na kimsingi, staili ya Lowassa ya kuvaa kofia ya pama ikaja kuigwa na viongozi wengine mfano wa John Pombe Magufuli.

Kofia ya pama kimsingi inavaliwa na mfugaji, mkulima na hata mafundi, iwe ujenzi au magari, hivyo, ni ya tabaka la Wakulima, wafugaji na wafanyakazi. Hao ndio wapiga kura walio wengi.

Lowassa alijua hata njia gani ni nzuri kwa msafara wake kupita. Kuna wakati akiwa waziri mkuu, akitokea uwanja wa ndege kwenda nyumbani kwake, Lowassa alipita barabara za Kigogo na Kawawa.

Hivyo, kupitia Magomeni, Kinondoni Mkwajuni na Kinondoni -Kwa Manyanya

## Kumbukizi

## Kwanini Lowassa alikuwa jive kwenye maji?

Inatoka Uk. 17

pia.

Wananchi hawakuzoea. Wamezoea waheshimiwa wakipita Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, hivyo, Lowassa akaacha gumzo njia nzima. Na maswali pia. Tena msafara haukupita kwa kasi. Waliomwona walisema; “leo tumemwona Lowassa!”

**Ambao hawakumwona waliuliza;**  
“Ni kiongozi gani kapita hapa leo?”

Wenye majibu walikuwa wengi. Hapo Edward Lowassa wala hakutumia nguvu nyingi kujitangaza.

**Swali:** Kwanini isemwe kuwa Lowassa alikuwa ‘bingwa’ wa siasa za mikakati?

**Jibu:** Mwanasiasa hupaswi kutengeneza maadui, bali jitahidi hata wale maadui zako kisiasa wawe rafiki zako.

Kwamba mwanasiasa uwaheshimu pia wakosojaji wako. Ni wenye kukutakia heri.

Lowassa aliwajua kwa majina wachambuzi na wanasafu wote wa magazetini wenye kuchambua siasa za Tanzania. Nilikuwa mmojawapo.

Nilichambua mazuri yake na nilimkosoa pia. Kuna wakati, katika kumkosoa kwangu Lowassa, Mhariri wa Rai (Sasa marehemu) alianza, kwa woga na kutojiamani, kuandika upya nilichokiandika. Hapo nikaacha kwa hiyari kuandikia Rai.

Kuna siku nikapokea simu ya Edward Lowassa akiwa ziarani nje ya nchi. Akaniuliza; “Maggid, mbona sioni makala zako siku hizi?”

Nikamjib, “Mheshimiwa Lowassa, kuwa nimeamua kupumzika kuandika na kuwa msomaji wa Rai.

Huyo ndiye Edward Lowassa ambaye pia aliona umuhimu wa kukoselewa na kujisahihisha.

Kwenye uhai wake, nimepata bahati



Lowassa akisalimiana na Misengo Pinda (kulia), ambaye alimrithi nafasi ya uwaziri mkuu baada ya kujiuzulu.

ya kukutana ana kwa ana mara mbili na Edward Lowassa.

Nakumbuka kuzungumza naye kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2015. Kwenye mazungumzo yangu yale ya ana kwa ana, na ya mwisho nikiwa na Edward Lowassa, kuna mapya niliyojifunza.

Mchana mmoja kwenye ofisi ndogo ya Lowassa, na isiyu na mbwembwe nyingi, nilikaa pamoja na aliyekuwa msaidizi wake, kaka yangu Aboubakar Liongo. Ni pale eneo la Mikocheni.

Kichwani nilikuwa na maswali kadhaa kwa Lowassa. Nilikuwa na hamu pia ya kusikiliza uzofu wake.

Nilimwona Lowassa akiwa ni mtu makini sana. Aliongea kama mtu aliye na mzani wa kupima maneno mdomoni mwake.

Hakuacha kuingiza utani pia. Akamwulizia hata rafiki yake wa miaka mingi; “Vipi Edmund, bado anaishi Mbezi?”

Kanali Edmund Mjengwa (Marehemu) alipata kuwa Mbunge wa Mbarali na rafiki pia wa Edward Lowassa. Edmund ni kaka yangu.

Kupitia mazungumzo yetu, nilimwona Lowassa aliyeyaona makosa ya upinzani kuingia kwenye mtego wa kufikiria zaidi njia za mkato za kuingia bungeni na kukamata dola.

Endelea Uk. 19

## **Kwanini Lowassa alikuwa jiwe kwenye maji?**

*Inatoka Uk. 18*

Hivyo, katika ajenda ile ya ndani ya CCM ya vita dhidi ya mafisadi, ambayo ilikuwa moja ya swali langu kwake, Lowassa aliona haja ya uwepo wa vita dhidi ya mfumo unaosababisha ufisadi.

Kwamba vyama vya upinzani vimeonesha kukosa mikakati thabiti ya kuutumia vyema udhaifu ule wa CCM kwenye kuanza kwanza na kupambana na mfumo.

Hivyo basi, kwa maono ya Lowassa, vyama vya upinzani vilionesha kuwa na udhaifu wa ndani ya vyama hivyo. Kuwa navyo ni vya kawaida, na kuwa mengine yaliyo ndani ya CCM yamo pia ndani ya vyama vya upinzani, na wakati mwingine kwa kiwango kikubwa zaidi.

Na kibaya, kama ilivyo kwa CCM, navyo vinapokumbwa na migogoro ya ndani, basi, hukimbilia kukanusha, kuwa havina migogoro. Vinakosa ujasiri wa kukiri upungufu na hivyo kuwa na fursa ya kujirekebisha.

Navyo pia vina wenye kuziba masikio na kufumba macho kwa matatizo yaliyo dhahiri. Ni yaleyale.

Kwamba hiyo ni hali ya kusikitisha kwa wapenda mageuzi ya kimsingi hapa nchini, lakini, kama navyo vina dhamira za dhati za kusaidia kuwakomboa Watanzania, basi, vina nafasi ya kujirekebisha. Kwa alivyoona Lowassa.

### **Kuhusu Urais?**

Nilimwuliza; Kwa Lowassa aliamini kwenye siasa kuna wanaotangaza nia na wanaotangaziwa nia.

Kwake, kundi hilo la pili ni la walioshindwa kabla ya kuanza. Na kwamba, kila Chama kina utamaduni wake, kwa CCM, aliye muhula wa kwanza kwenye urais wake, huachwa amalaze ya pili. Akitaka wa tatu ataanzisha ugomvi tu. Hatoshinda.

### **Hitimisho:**

Kwa hakika, Edward Lowassa kisiasa alikuwa kama mawimbi ya jiwe. Ni jiwe

linapotumbukia majini kwamba huacha mawimbi.

Na jiwe likiwa kubwa, basi, mawimbi yake huwa mengi na makubwa pia. Kila alipotua mwanasiasa Lowassa kulionekana uwepo wa mawimbi mengi na makubwa.

### **Iliashiria nini?**

Tafsiri ni nyingi, lakini, kwa wanasiasa makini waliodhamiria kupambana na Lowassa walikuwa na swali la msingi la kujiuliza; je, unafanyaje kama kuna mawe mengine makubwa yanayoshabihana ( kuungana) na ya Lowassayanapoanza kutumbukia majini?

Mwingine angedhani, kuwa busara ni kupunguza ukubwa wa jiwe kabla halijawa kubwa.

Maana, kwa mwanasiasa aliyepambana na Lowassa, angependa 'jiwe Lowassa' liwe kama changarawe. Kwamba ikitumbukia majini haiachi mawimbi.

Lakini, kazi ya kuliponda jiwe Lowassa ili libaki kuwa changarawe ilihitaji nyundo kubwa.

Na kwa walio ndani na nje ya CCM waliotaka kuifanya kazi hiyo, walijiuliza mara mbili - mbili. Waliujua ugumu wake.

*Apumzike Kwa Amani, Edward Ngoyai Lowassa.*



*Edward Lowassa akisalimiana na Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe (kulia). (Picha kutoka MwanaHALISI Online)*

# Ivory Coast bingwa Afcon...



Timu ya Taifa ya Ivory Coast, jana iliibuka mabingwa wapya wa michuano ya kabumbu Afrika, baada ya kuwabwaga Nigeria kwa mabao 2-1. Katika picha hii, shabiki wa Ivory Coast (kulia), akifurahia jambo na mpinzani wake wa Nigeria. Mpira ni udugu, mpira ni raha. Pambazuko tunawapongeza washindi. (Picha na Mtandao wa X wa Afcon23).

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

